

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Mahakama,

S. L. P. 1419,

53103 MBEYA.

Simu: (025) 252503566

Nukushi: (025) 252502958

Barua pepe: rbcmbeya@pccb.go.tz

Wavuti: <http://www.pccb.go.tz>

TAARIFA KWA UMMA

MBEYA - JULAI 14, 2020

ACHUGUZWA NA TAKUKURU WILAYA YA KYELA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya inamchunguza Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kyela Bw. Hunter Albert Mwakifuna ambaye ni mgombea wa kiti cha Ubunge Wilaya ya Kyela pamoja na wajumbe wa CCM kata ya Makwale kwa kosa la kushawishi wajumbe ambao ni wapiga kura kupitisha jina lake wakati wa kura za maoni kinyume na Kif cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Mgombea huyo pamoja na wajumbe hao walikutwa na maafisa wa TAKUKURU Wilaya ya Kyela wakiwa wanafanya kikao kilichoitishwa na mgombea huyo katika shamba la Kakao kinyume na taratibu kwa lengo la kuwashawishi wajumbe hao ili wapitishwe jina lake katika kura za maoni.

Uchunguzi wa tuhuma hii bado unaendelea. Taarifa kamili itatolewa baada ya uchunguzi huu kukamilika.

WITO KWA WANANCHI

Tunawapongeza wananchi wa Wilaya ya Kyela na mkoa wa Mbeya kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Taasisi yetu katika mapambano dhidi ya rushwa.

Tunawasihi kuendelea kuwasilisha taarifa za wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwa kupiga simu namba 113, kuandika ujumbe mfupi wa maneno

kwenda namba 113 au kubonyeza *113# na kufuata maelekezo Huduma hizi zinapatikana BURE kwa mitandao yote ya simu.

IMETOLEWA NA:

JULIETH MATECHI
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA
